1013/1
MTIHANI WA MWIGO
MACHI/APILI/2018
MUDA : SAA 2

JINA LA MTAHINIWA_______________________________________________DARASA____________

NAMBARI____________________________________TAREHE___________________________

MAAGIZO

1. Andika jina lako, tarehe na darasa kwenye nafasi ulizoachiwa.
2. Mtihai huu una sehemu NNE MUHIMU; Insha, Ufahamu, Mtumizi ya lugha na Sajili ya lugha .ni muhimu ufwate maaagizo yote mwanzoni mwa kila sehemu.
3. Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.
4. Usitoe karatasi yeyote katika kijitabu hiki.

**Kwa matumizi ya mtahini**

| **sehemu** | **Swali** | **upao** | **Alama** |
|---|---|---|---|
| **1** | | | |
| **2** | | | |
| **3** | | | |
| | | | |
| **4** | | | |
| | | | |

**SEHEMU YA KWANZA INSHA:**
(ALAMA 20)

1 Andika insha isiyo pungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazwo:

a) Wewe ni mgeni wa heshima katika sherehe za mahafali chuoni. Andika hoyuba utakayo itoa siku ile.

b) Wanafunzi hawafai kuruhusiwi kuwa na rununu shuleni. Jadili.

c) Andika insha itakayodhuhulisha ukweli wa methali "Ajizi ni nyumba ya njaa'.

d) Tunga kisa cha kuvutia katikachomaliza kwa maneno haya: …………………………..ingawa sikutaka kuamini ukweli huo, hatimaye ilinibidi.

**SEHEMU YA PILI; UFAHAMU (ALAMA20**

2. Soma sehemu ifuatayo kasha ujibu maswali.

Kiswahili bila shaka ni mojawapo ya lugha za kimataifa zinazozungumuzwa ulimwenguni lakini ni kinaya kua sisi wenyeji wa eneo la Africa Mashariki, ambao ni kitovu cha lugha hii, tumekua tukinyonga rasilmali hii kwaukatili mkubwa.

Ni aibu iliyoje kwetu sisi tunapokitumia Kiswahili kiholela bila kuzingatiakaida zake huku tukijidanganya kua sisi ni mahiri tuapokiporomosha Kiingereza kwa usinafun mkubwa. Jinsi tunavyo kitema kimombo kisawasawa, kwa nini hali hii tusiizingatie katik hii lugha yetu tunu? Isitoshe, tunapozungumuza Kiswahili tunajitia hamnazo. Hebu fikiria!Baadhi ya wageni kutoka nchi za ulaya Marekani wameuliza baadhiya wafrika walioenda kusoma nci zao kwa kimako, iwapo Waafrika wana lugha zao. Wengine, waliopata fursa ya kutembea eneo hili wametambua utamu wake, wakajifunza na kukitumia Kiswahili kwa njia inayopendeza. Lisha ya hayo, wamejistawisha miongoni mwao kukawa na walimu wa lugha hii ilhali tumesahau kutumia raslimali yetu kujinufaisha.

Tunazidi kukitia kitanzi Kiswahili. Kupitia uchapishaji wa magazeti yetu. Bei ya magazeti la Kiswahili inaashiria uduni wake. Kiasi cha habari kinachochapishwa na kukusanywa katika gazeti hili ni finyu sana n kuhidhilisha ukosefu wa utaalamu ukilinganishw na kiingereza. Kwa sabau hii, msomaji wa gazeti atanunua lile la baei ghali- lenye habari kamili kuliko vitu nusunusu.Chakuudhi zaidi ni kua baadhi ya habari za magazeti ya Kiswahili hujikuta katika masuala ya kijamii kwa kiasi

kukubwa na kuyapa kisogo au kugusiagusia tu mambo kuhusu uchumi, siasa, jiografia na dini. Hakuna mazito kuhusu matangazo ya biashara, hakuna habari ya vifo, hakuna habari za ajira na kadhalika.si ajabu wakati mmoja niliulizwa mtaani, ' Hili gazeti ulilo nalo umenunulia babu yako?" swali hili lilinijulisha kua kasumba ya watu wengi imejengwa na mtindo wa wakati mrefu wa kuchapicha magazeti kwa njia hii, hivi kwamba magazeti ya Kiswahili yanafaa kusomwa na wazee, na labda wale wlioshidwa na masomo shuleni.

Si magazetini tu ambapo ugandamizaji huu unafanywa bali hata katika vyombo vingine vya habari. Sielewi sababu ya baadhi ya vipindi takribani vyote vya runinga viwasilishwe kwa kiingereza harafu tarifa iletwe mara mioja kwa Kiswahili katika siku nzima.Ningependa kuona kukiwa na uninga yenye kutangaza vipindi vyote kwa Kiswahili kama zilivyo baadhi ya redio. Sijui kama waandalizi wa vipindi hivi vya runinga wana habari kuwa kuna talanta nyingi katika tamasha za drama kwa vyuo na shule nchini. Watangazaji ni mwongoni mwa wenye kutweza Kiswahili kwa kutoa mahojiano kupitia runinga kwa kiingereza hasa katika masuala mbalimbali ya kitaaluma. Mbona wasialike katika studio wataalamu ambao wanaweza kueleza maswala nyeti kuhusu wananchi kw kutumia Kiswahili?

Serikali imelegea kwa kutochukua hatua zaidi ya ilivyofanya. Baadhi ya nci zetuzingali katika hali ya eti, mara eh! Mara oh! Ni vyema kiwhili kifanye lugha rasmi kote katika eneo hili na wanasiasa wachukue mstali wa mbele kukitimia Kiswahili katika mikutano yao na katika bunge tukianza na rais pamoja na myungo wake.

Tope lote tulilo likanyanga tunalipangusia katikakiswahili chetu. Eti mtu akizungumza Kiswahili njiani aali anasemwa kua mjanja mwenye nia ya kukwepua miliki ya wenyewe. Mtazamo huu pamoja na uke kwmba msemaji wa lugha hii hajasoma unafaa kuzikwa katika kaburi la sahau kwani baadhi ya vyuo vikuu vya Kenya na hata za Marekani na Ulaya, ligha hii inafunzwa.

Kisiki kikuu huchupikua katika sector ya elimu. Iwapo kingereza kitatumiwa kufundisha masomoyote ilhali somo moja lifunzwe kwa kiswahiliutatarajia miujiza gani? Itakua vigumu sana kunishawishi kua serikali inania jema kw Kiswahili. Ndiyo sababu katika baadhiya shule, wanafunzi wanaokitumi a Kiswahili huadhibiwa sawa na wanaozitumia lugha nyingine za kiafrika. Ningependa kushauri hali hii ifikiriwe upya kwa kina na washika dau ili sera zinazohusu elimu zikarabatiwe.

Joakim Chisano wa Msumbiji aliyekuwa mwenyekiti wa jumuiya ya Africa ni mfano mzuri sana wa kuingiza na viongozi wetu. Katika kongamano lilofanyika kule Addis Ababa, uhabeshi mwaka 2002

alitumia Kiswahili kwa mshangao wa wngi alipohutubia kikao cha jumuiya hii. Ang jamuhuli ya Muungano wa Watanzania imetuonyesha nia na hivyo kutulazimu wengine tuone njia. Kupitiswa kwa Kiswahili kama lugha mojawapo ya zile rasmi katika vikao vya jumuiya ya Africa ni hatua mwafaka katika kutambua dhima ya lugha hii.

(a) Ipe habari hi kichwa kinachfaa. (alama1)

(b) Ni mambo yapi yanayoshangaza mwandishi kuhusu utumiai wa Kiswahili na wageni. (alama3)

c) Taja njia tatu zinazoonyesha kuwa vyombo vya habari vimedidimiza Kiswahili.(alama6)

(c) Ili kukiimarisha Kiswahili katika eneo la Africa Mashariki, mwandaishi anapendekezaserikali au watawala wa kisiasa wafanye nini? (alama4)

(d) Taja maneno matatu ambayo yametumika katika ufahamu ili kuleta dhana ya kididimiza Kiswahili. (alama 3)

(e) Eleza maana ya maneno au vufungu vya maneno yafuatayo:

(i). Akilonga.

(ii). Tunavyo kitema kimombo.

(iii). Kukwepua milki.

**SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA KUGHA(ALAMA50)**

3(a) kanusha.

Walikuwa wakicheza na kuimba. (alama1)

(b) Andika umoja wa sentence hii (alama2)

Wao walitusaidia sisi.

(c) Tumia 'o' rejeshi ys mwisho katika sentensi hii (alama1)

Mtu amabaye hula hunenepa

(d) Andika ukubwa wa sentnsi hii (alama2)

Paka huyu amekua mwizi

(e) Taja na ueleze viambishi vinavyoonyesha mahali: (alama3)

i)

ii)

iii)

(f) Andika mfano mmoja wa neno la Kiswahili lenye muundo wa irabu pekee.(alama1)

(g) Tunga sentence moja ukitimia: (alama1)

(i). Kielezo cha nomino

(ii). Kivumishi cha nomino.

(h) Mbali na 'ki' ya masharti, tunga sentensi mbili tofauti ukitumia viambishi vinavyoashiria masharti. (alama2)

i.

ii.

(i) Ainisha sentensi hii (alama2)

Tunda tamu liliwa leo.

(j) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii

Ananikimbilia (alama2)

i.

ii.

(K)a Andika matumizi mawili ya kinyota (alama2)

i.

ii.

(b) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya paradesi. (alama1)

______________________________________________

______________________________________________

k) Bainisha jinsi 'Ni' iliyotumika katika sentensi hizi. (alama1)

i. Waliingia darasani

______________________________________________

______________________________________________

ii. Huyu ni mwalimu wetu.

______________________________________________

______________________________________________

(m) Bila kubadiliah maana andika sentensi hii kwa njia mbili tofauti. (alama2)

Matunda yalikua ndani ya kikapu.

i. ______________________________________________

______________________________________________

ii. ______________________________________________

______________________________________________

(n) Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi: (alama3)

Ameadhibiwa

______________________________________________

______________________________________________

(o) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kufanyisha (alam1)

Mama alimfanya mtoto alie

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

(p) Bainisha vishazi katika sentensi hii. (alama1

Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

(q) Tunga sentensi moja ukitumia 'ki' ya vitenzi vinavyofanyika wakati mmoja.(alam1)

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

( r) Tunga sentensi ukitumia neno <u>maadam</u>. (alama1)

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

4 (a) Mtu anayehamia nchi isiyokuwa yake na kufanya makazi ya kudumu huko alikohamia huitwa setia au________________________________.(alama1)

(b) Msichana aliyevunja ungo lakini hajadewa huitwaje_________________________ (alama1)

(c) Chepeo ni vazi lipi?________________________________________________________ (alam1)

(d) Kandawala hufanya kazi ipi?__________________________________________________(alam1)

e) Uzito wa bidhaa hupimwa kwa kutumia ratili au_________________________________ (alama1)

(f) Jiriwa au kibanio ni kifaa kipi? _____________________________________________ ( alama1)

(g) Ni ugonjwa upi huumfanya mbwa kushikwa na wazimu na anapomuuma binadamu huambukiza ugonjwa huu?________________________________________________________________(alama1)

(h) _______________________________ni makao ya nyuki.(alama1)

(i) Toa neno moja kwa maelezo yafuatayo

Ndege mmoja wenye kucha ndefu na kali na mabaye chkakula chake kikuu ni mzoga(alam1)

(J) Huyu ni mdudu yupi?

Kupe______________________________________________________________(alama1)

(K) Angalabu umbo la mkate ni____________________________________________ (alama1)

(l) ____________________________________ni kiogo cha mwili ambacho husukuma damu ili ienee kwa kupitia kwenye miships(alam1)

(m) Haya ni malipo gani

Bahashishi ______________________________________________________________

(n) Fafanua msimu huu.(alama1)

Ukame_________________________________________________________________

(O) Baruji ni ala ipi ya muziki_____________________________________________________(alama1)

(p) Taja kisawe cha dhiki_____________________________________________(alam1)

(q) Tegua

Hushidana wakifuatana. (alama1)

___________________________________________________________________________

(r) _________________________________________ni sayari iliyo na pete tatu maridadi sana.(alama)

(s) Andika kwa tarakimu

Millionikumi na tatu, hamsini na tatu elfu mia tisa na hamsini. (alama1)

________________________________________________________

(t) ______________________ ni tamko linalotumiwa na mtu aliye na nia ya kutenda jambo fulani (humaanisha mungu akipenda) (alama1)

SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (ALAMA 1O)

5. Eleza umuhimu wa kusanifisha lugha. (alam10)

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

______________________________________________________________